# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)

# UTEKELEZAJI WA MTAALA ULIOBORESHWA WA ELIMU YA SEKONDARI: WAJIBU WA MTHIBITI UBORA WA SHULE

*Dkt. ANETH A. KOMBA*
Mkurugenzi MKUU (TET)
23 NOVEMBA, 2024

# DONDOO

- Utangulizi-Kuhusu TET
- Muundo wa Elimu
- Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Sekondari
- Wajibu wa Mthibiti Ubora wa Shule
- Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Ualimu
- Wajibu wa Mthibiti Ubora wa Shule
- Hitimisho

# Utangulizi

- **Kuhusu TET na Majukumu yake**

  - Taasisi ya Elimu Tanzania ni Taasisi ya umma iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 13 ya Mwaka 1975 (Sura ya 142 Marejeo ya 2002).

# Utangulizi…

## Majukumu ya TET:


- Kubuni, kuandaa na kuboresha Mitaala ya Ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mitaala;
- Kuandaa vifaa saidizi vya kutekeleza mtaala na kuhakiki ubora wa vifaa vinavyolengwa kutumiwa katika Ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu;

# Utangulizi...

- Kutoa mafunzo kwa watekelezaji na wasimamizi wa mitaala wakiwemo walimu, Maafisa Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu wa Halmashauri na Mikoa ili waweze kutekeleza mitaala kwa ufanisi; na
- Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya mitaala, ufundishaji, ujifunzaji na ubora wa elimu kwa ujumla.

# Muundo wa Elimu

- Muundo nyumbufu (**A flexible education system**) umeandaliwa kwa kuzingatia maoni ya wadau, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023, nyaraka mbalimbali na uzoefu kutoka nchi nyingine.


Elimu bila Ukomo na Vyeti vya Ubobezi
Elimu ya Ufundi Stadi (Vocational Education)
Maisha ya Kazi
Elimu ya Jumla ya Juu (TCU)
(General Higher Education)
Miaka 3+
(Umri miaka 18+)
Elimu ya Amali ya Juu
(Technical Higher Education)
(NACTVET)
Miaka 3+
(Umri Miaka 19+)
Maisha ya Kazi
Elimu ya Ufundi Stadi (Vocational Education)
Elimu bila Ukomo na Vyeti vya Ubobezi
Sekondari Hatua ya Juu
Elimu ya Jumla
Miaka 2
(Umri Miaka 16-17)
Elimu ya Amali Sanifu
Miaka 3
(Umri Miaka 16-18)
Elimu ya Lazima
Sekondari Hatua ya Chini
Elimu ya Jumla
(General Education)
Miaka 4
(Umri Miaka 12-15)
Sekondari Hatua ya Chini
Elimu ya Amali
(Vocational Education)
Miaka 4
(Umri wa Miaka 12-15)
VETA kama Mwezeshaji
Elimu ya Msingi Miaka 6
(Umri Miaka 6-11)
(D1-D2) (D3-D6)
Elimu ya Awali
Mwaka 1
(Umri Miaka 5)
Elimu ya Malezi na Makuzi
Miaka 2
(Umri Miaka 3-4)
Ufunguo
Kuingia
Kutoka
Kuingia /Kutoka
Elimu bila Ukomo

# Maboresho Muhimu katika Ngazi ya Elimumsingi

- Muda wa Elimu ya Msingi umepunguzwa kutoka miaka saba (7) hadi miaka sita (6)
- Muda wa Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini na Sekondari Hatua ya Juu umeendelea kuwa miaka minne (4) na miaka miwili (2) mtawalia.
- Elimu ya Msingi na ile ya Sekondari Hatua ya Chini zimekuwa za lazima hivyo kuifanya elimu ya lazima (*compulsory basic education*) kuwa miaka kumi (10).

# Maboresho muhimu katika Ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini

- Elimu ya Sekondari hatua ya chini imegawanyika katika mikondo miwili:
  - ✓ Mkondo wa Elimu ya Amali
  - ✓ Mkondo wa Elimu ya Jumla

# Maboresho Muhimu katika Ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini

## Sekondari Hatua ya Chini-Mkondo wa Amali

- Utekelezaji wa umeanza Januari, 2024.
- Mkondo huu ni nyumbufu unaomwezesha mwanafunzi kurudi mkondo wa jumla kwa kujiunga na Kidato cha Tano au kuendelea na mafunzo ya Ufundi Sanifu bila kikwazo.
- Mwanafunzi katika mkondo huu anajifunza masomo ya fani yanayotolewa kwa kutumia mtaala wa VETA pamoja na masomo ya jumla yanayotolewa kwa kutumia mtaala wa TET.

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **UHANDISI**<br>Electrical Installation, Motor Vehicle Mechanics; Welding and Metal Fabrication; Painting and Sign Writing; Carpentry and Joinery with Metal work; Masonry and Brick Laying; Plumbing and Pipe Fitting; and solar Power Installation | Fani | Mathematics | i. Mathematics, Economics and Business Studies and (MEBu).<br>ii. Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM)<br>iii. Physics, Mathematics Computer Science (PMCs)<br>iv. Business Studies, Economics and English Language (BuEL) |
| | Technical Drawing | Business Studies | |
| | Computer application with CAD | English Language | |
| | Life Skills | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | Engineering Science | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **UKARIMU NA UTALII**<br>Food Production; Food and Beverages Services; House Keeping; Front Office Operations; Tour Guide | Fani | Mathematics | i. Mathematics, Economics and Business Studies (mebU)<br>ii. Tourism, English Language and French (TLF)<br>iii. Business Studies, English Language and French (BuLF)<br>iv. French, English Language and Economics (FLE)<br>v. Business Studies, Econnomics and English Language (BuEL)<br>vi. Business Studies, Economics and French (BuEF) |
| | Tourism for Hospitality | Business Studies | |
| | Life Skills | English Language | |
| | Computer Application | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | French/Arabic/ Chinese | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **KILIMO/MIFUGO**<br>Crop Production, Horticulture Production, Animal Health and Production, and Meat Processing | Fani | Mathematics | i. Business Studies, Economics and English Langauage (BuEL)<br>ii. Agriculture, Biology and Economics (ABE)<br>iii. Biology, Mathematics na Agriculture (BMA)<br>iv. Mathematics, Economics and Business Studies (MEBu)<br>v. Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM) |
| | Life Skills | Business Studies | |
| | Computer Application | English Language | |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | Agriculture Biology | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **SANAA NA MAONESHO**<br>Music Performance, Music Sound and Technology, Acting, and Ngoma | Fani | Mathematics | i. Business Studies, Economics and English Language (BuEL)<br>ii. English Language, Music (LChMu) and any other foreign Language like English Language, French and Music.<br>iii. Business Studies, Economics and any other foreign Language/French/Chinese/ Arabic<br>iv. English Language, French and Theatre Arts (LFT) and any other foreign languages. |
| | Life Skills | Business Studies | |
| | Computer Application | English Language | |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | French/Chines/ Arabic Language | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **MICHEZO** Football, Netball, and Track Event | Fani | Mathematics | i. Business Studies, Economics and English<br>ii. Business Studies, Economics and any other foreign language<br>iii. French, English Language and Sports (FLS)<br>iv. English Language, Chinese and Sports (LChS) |
| | Life Skills | Business Studies | |
| | Computer Application | English Language | |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | French/Chines/ Arabic Language | |
| | | | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **TEHAMA**<br><br>Graphic Design, and Computer Programming | Fani | Mathematics | i. Business Studies, Economics and English Language (BuEL)<br>ii. Economic, Computer Science and Mathematics (ECsM)<br>iii. Business Studies, Mathematics and Computer Science (BMC)<br>iv. Mathematics, Economics and Business Studies (MEBu) |
| | Life Skills | Business Studies | |
| | Computer Application | English Language | |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | French/Chinese/ Arabic Language | |
| | | | |

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Amali

| FANI | Mtaala wa VETA | Mtaala wa TET | TAHASUSI |
|---|---|---|---|
| **USHONI**<br><br>Leather Goods and foot wear, Design sewing and cloth Technology, Handloom and Weaving | Fani | Mathematics | i. Mathematics, Economics and Business Studies (MEBu)<br>ii. Business Studies, Economics and English Language (BuEL)<br>iii. Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM) |
| | Life Skills | Business Studies | |
| | Computer Application | English Language | |
| | | Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | French/Chinese/ Arabic Language | |
| | | | |

# Wajibu wa Wathibiti Ubora wa Shule

- Kuuelewa muundo wa elimu ulioboreshwa, kusaidia kutoa uelewa wa muundo huo kwa wadau mbalimbali katika maeneo yetu, ikiwezekana kuuchapa (print)/ na kuziomba shule kuuchapa na kuubandika sehemu maalumu ambayo itawawezesha walimu, wanafunzi na wadau wengine kuurejelea mara kwa mara.

# Wajibu wa Wathibiti Ubora wa Shule

- Kutoa mafunzo ya mtaala ulioboreshwa kwa watekelezaji wa mtaala katika maeneo yetu.
- Kufanya ufuatiliaji katika shule zinazotoa mkondo wa amali na kujihakikishia kuwa mitaala inatekelezwa kadiri ya mpango wa utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa.
- Kujiridhisha iwapo watekelezaji wa mtaala wanafahamu utaratibu sahihi wa kutoa elimu ya sekondari ya amali na kutoa afua stahiki iwapo kuna uhitaji (kutoa elimu husika au kuwasiliana na taasisi husika).

# Wajibu wa Wathibiti Ubora wa Shule...

- Kujiridhisha iwapo wanafunzi na wazazi wanaelewa juu ya Elimu ya Amali.
- Kutumia zana *(tool)* iliyoandaliwa na NACTVET kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masomo ya Amali katika shule husika (miundombinu, rasilimaliwatu, ufundishaji na ujifunzaji wa darasani nk).
- Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masomo ya Jumla katika shule husika (miundombinu, rasilimaliwatu, ufundishaji na ujifunzaji wa darasani nk)

# Wajibu wa Wathibiti Ubora wa Shule...

- Kujiridhisha na uwepo wa vifaa vya utekelezaji wa mtaala kwa fani inayotolewa pamoja na masomo ya jumla na kama havipo kuwasiliana na TET kwa haraka.
- Kuijengea uwezo timu ya uthibiti ubora wa shule ya ndani ili iweze kusimamia ubora wa elimu ya amali inayotolewa shuleni.
- Kujadiliana na watekelezaji wa mitaala juu ya utatuzi wa changamoto iwapo zipo.
- Kufanya tafiti tatuzi ili kutoa ushauri utakaosaidia kuboresha utekelezaji wa elimu ya amali.

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini-Mkondo wa Jumla

- Utekelezaji utaanza Januari, 2025.
- Mtaala ulioboreshwa Mwaka 2023 Sekondari Hatua ya Chini una masomo 27.
- Masomo matatu ya *Additional Mathematics, Literature in English* na Fasihi ya Kiswahili yanafundishwa kuanzia Kidato cha Tatu.
- Masomo 24 yanafundishwa kuanzia Kidato cha Kwanza.

# Masomo katika Ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Additional Mathematics | 10 | English Language | 19 | Bible Knowledge |
| 2 | Mathematics | 11 | Arabic Language | 20 | Fine Art |
| 3 | Physics | 12 | French | 21 | Music |
| 4 | Chemistry | 13 | Chinese | 22 | Sport Studies |
| 5 | Biology | 14 | Literature in English | 23. | Theatre Arts |
| 6 | Computer Science | 15 | Fasihi ya Kiswahili | 24 | Food and Human Nutrition |
| 7 | Agriculture | 16 | Historia ya Tanzania na Maadili | 25 | Textile and Garment Construction |
| 8 | Geography | 17 | History | 26. | Book-keeping |
| 9 | Kiswahili | 18 | Elimu ya Dini ya Kiislamu | 27 | Business Studies |

# Sekondari Hatua ya Chini- Mkondo wa Jumla

- Mkondo huu una **michepuo 11** ambayo

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Sayansi | 7 | Sayansi ya Jamii |
| 2 | Kilimo | 8 | Sanaa |
| 3 | Michezo | 9 | Upishi |
| 4 | TEHAMA | 10 | Ushoni |
| 5 | Biashara | 11 | Lugha |
| 6 | Muziki | | |

## SEKONDARI YA CHINI (Elimu ya Jumla)



# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mkondo wa Jumla

- Idadi ya masomo ya lazima katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini imepungua kutoka saba (7) hadi sita (6).
- *Biology* na *History* yamekuwa ni masomo chaguzi. Maudhui muhimu ya somo la *Biology* yamejumuishwa kwenye somo la Sayansi Elimu ya Msingi. Maudhui ya Somo la Historia yanafundishwa katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mkondo wa Jumla

- Tumeimarisha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuimarisha umahiri wa kinadharia na kimatendo na sasa Mwanafunzi anapaswa kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali, kufanya kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazi mradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira yake kwa lengo la kukuza ubunifu.

# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mkondo wa Jumla

- Tumeimarisha upimaji endelevu, wezeshi na tamati kwa kutumia zana na mbinu zinazopima nadharia na vitendo kwa kuzingatia mtaala wa ujenzi wa umahiri.

- Ili kujenga stadi za **Ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo** tumeimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mbinu zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi uwezo wa kufikiri, kutafakari, kubuni na kutatua matatizo.

# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya chini Mkondo wa Jumla

- Tumeunganisha masomo ya Uraia, *Civics* na Historia ya Tanzania kuwa somo moja linaloitwa Historia ya Tanzania na Maadili na somo hili linafundishwa kwa Kiswahili katika ngazi zote.

- Tumeongeza msisitizo kwenye maadili na uzalendo kwa kuzingatia elimu ya imani ya dini katika ngazi zote za elimu.

# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mkondo wa Jumla

- Somo la *Information and Computer Studies* limebadilishwa jina na kuwa *Computer Science*.

- Somo la *Commerce* limeandaliwa upya ili liweze kumwandaa mhitimu kutumia ujuzi kufanya biashara ndani na nje ya Tanzania. Somo hili ni la lazima katika ngazi ya Sekondari Hatua ya Chini na limebadilishwa jina kuwa *Business Studies*.

# Maboresho katika Ngazi ya Sekondari ya Chini Mkondo wa Jumla

- Ili kukuza stadi ya Karne ya 21 ya kushirikiana tumechopeka masuala yanayohusu mitazamo na matendo jumuishi katika mitaala ya masomo yote kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali, hivyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanafundishwa katika madarasa jumuishi kwa kadri itakavyowezekana.
- Programu ya ualimu wa elimu maalumu imeboreshwa ili kuwajengea wahitimu umahiri wa kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na mahitaji yao.

# Wajibu wa Mthibiti ubora

- Kutoa elimu ya mitaala iliyoboreshwa kwa watekelezaji wote wa mitaala katika eneo lako (wawezeshaji).
- Kuhamasisha MEWAKA katika Mikoa/Halmashauri zetu.
- Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mitaala ili kujiridhisha kuwa inatekelezwa kama ilivyopangwa mfano masomo katika michepuo, utekelezaji wa vipindi vya dini na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundisha Somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

# Wajibu wa Mthibiti ubora

- Kufuatilia na kuhakikisha kuwa mitaala inatekelezwa kwa kadiri ya mpango wa utekelezaji wa mitaala uliowekwa na serikali.
- Kusimamia viwango vya elimu inayotolewa kwa kuzingatia maboresho ya mitaala yaliyofanyika
- Kujiridhisha iwapo walimu wanatumia zana za upimaji zinazozingatia ujenzi wa umahiri (CBC).

# Wajibu wa Mthibiti ubora

- Kuzingatia juu ya uwepo wa vifaa ya kufundishia na kujifunzia na kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanywa kwa kuzingatia ujumuishi na CBC na kuwasiliana na TET iwapo kuna uhitaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na mafunzo.
- Kuhamasisha MEWAKA katika Mikoa/Halmashauri zetu, matumizi ya Maktaba Mtandao na LMS.

# Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu

- Utekelezaji utaanza Julai, 2025.
- Mtaala ulioboreshwa wa Mwaka 2023 Sekondari Hatua ya Juu umebainisha masomo 30.
- Masomo 25 ni mwendelezo wa masomo kutoka Kidato cha I-IV.
- Masomo matano yanaanzia Kidato cha Tano: ***Economics, Academic Communication, Tourism, Literature in English*** **na Fasihi ya Kiswahili**.
- Masomo mawili ni ya lazima ambayo ni **Historia ya Tanzania na Maadili** na ***Academic Communication.***

# Masomo katika mtaala ulioboreshwa Mwaka 2023 Ngazi Sekondari Hatua ya Juu

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Basic Applied Mathematics | 11 | Accountancy | 21 | Food and Human Nutrition |
| **2** | Advanced Mathematics | 12 | Business Studies | 22 | Textile and Garment Construction |
| **3** | Chemistry | 13 | Economics | 23 | Music |
| **4** | Biology | 14 | English Language | 24 | Sport Studies |
| **5** | Physics | 15 | **Literature in English** | 25 | Fine Art |
| **6** | Computer Science | 16 | Kiswahili | 26 | Theatre Arts |
| **7** | Agriculture | 17 | **Fasihi ya Kiswahili** | 27 | History |
| **8.** | Geography | 18 | Arabic Language | 28 | **Historia ya Tanzania na Maadili** |
| **9.** | Divinity | 19 | French | 29 | **Academic Communication** |
| **10** | Elimu ya Dini ya Kiislamu | 20 | Chinese Language | 30 | **Tourism** |

# Maboresho ya Mitaala…
# Sekondari Hatua ya Juu

- Kuanzisha somo jipya la lazima katika hatua ya Kidato cha Tano na Sita linalotilia mkazo wa kujenga uwezo wa kuwasiliana kitaaluma (*Academic Communication*).
- Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu imejikita kwenye masomo yaliyopangwa katika tahasusi kwa muda wa miaka miwili.

# Maboresho ya Mitaala…
# Sekondari Hatua ya Juu

- Idadi ya masomo ya tahasusi ni matatu lakini mwanafunzi anaweza kuchukua masomo manne kulingana na uwezo na malengo yake. Hii itamwongezea wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu.
- Idadi ya tahasusi imeongezeka kutoka **18** hadi **88** ili kuongeza fursa kwa wanafunzi kuchagua mchanganyiko wa masomo yanayoendana na utashi, uwezo na malengo yao ya maisha.

# Maboresho ya Mitaala…
# Sekondari Hatua ya Juu

- Mwanafunzi aliyefaulu somo la *Additional Mathematics* akiwa Sekondari Hatua ya Chini hatalazimika kusoma somo la *Basic Applied Mathematics* katika Sekondari Hatua ya Juu kwa sababu maudhui yake yanafanana.

# Tahasusi za Masomo…

| C: Business Studies | | Kada tarajiwa |
| --- | --- | --- |
| 23 | **Economics, Business Studies and Accountancy (EBuAc)** | Ualimu, Uchumi, Biashara, Uhasibu, Ugavi, Mipango, Uandishi wa Habari, Uhusiano (public relations), Rasilimaliwatu, Uthamini majengo na ardhi, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Banking and Finance |
| 24 | **Economics, Geography and Mathematics (EGM)** | Ualimu, Uchumi, Uhasibu, Upimaji ardhi, Urubani, Usanifu majengo, Ukadiriaji majenzi, Ugavi, Mipango, Archeology, Uandishi wa Habari, Uhusiano (public relations), Rasilimaliwatu, Uthamini majengo na ardhi, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Banking and Finance |
| 25 | **Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM)** | Ualimu, Uchumi, TEHAMA, Uhasibu, Upimaji ardhi, Ukadiriaji majenzi, Usanifu majengo, Ugavi, Mipango, Rasilimaliwatu, Uthamini majengo na ardhi, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Banking and Finance |
| 26 | **Business Studies, Accountancy and Computer Science (BuAcCs)** | Ualimu, Biashara, Uchumi, TEHAMA, Uhasibu, Ugavi, Mipango, Archeology, Uandishi wa Habari, Uhusiano (public relations), Rasilimaliwatu, , Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Banking and Finance |
| 27 | **Business Studies, Accountancy and Mathematics (BuAcM)** | Ualimu, Biashara, Uchumi, Uhasibu, Ugavi, Mipango, Uandishi wa Habari, Uhusiano (public relations), Rasilimaliwatu, Uthamini majengo na ardhi, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu |

# Tahasusi za Masomo…

| F: | Tahasusi za Michezo | Kada tarajiwa |
|---|---|---|
| 48 | **Biology, Food and Human Nutrition and Sports (BNS)** | Ualimu, Michezo, Afya, Lishe, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |
| 49 | **Sports, Arabic and English Language (SArL)** | Ualimu, Michezo, Ukocha, Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |
| 50 | **Fasihi ya Kiswahili, English Language and Sports (FaLS)** | Ualimu, Michezo, Ukocha Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |
| 51 | **French, English Language and Sports (FLS)** | Ualimu, Michezo, Ukocha Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |
| 52 | **Kiswahili, English Language and Sports (KLS)** | Ualimu, Michezo, Ukocha Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |
| 53 | **English Language, Chinese and Sports (LChS)** | Ualimu, Michezo, Ukocha Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia etc |

# Tahasusi za Masomo...

| H: Tahasusi za Elimu ya Dini | | Kada tarajiwa |
|---|---|---|
| 70 | **Islamic Knowledge, History and Geography (IHG)** | Ualimu, Archeology, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia, Falsafa etc |
| 71 | **Islamic Knowledge, History and Arabic (IHAr)** | Ualimu, Archeology, Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia, Falsafa etc |
| 72 | **Islamic Knowledge, History and English Language (IHL)** | Ualimu, Archeology, Ukalimani, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia, Falsafa etc |
| 73 | **Islamic Knowledge, History and Kiswahili (IHK)** | Ualimu, Archeology, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu, Utawala, Sheria, Sayansi ya Siasa, Diplomasia, Sosholojia, Falsafa etc |

# Wajibu wa wathibiti Ubora…

- Kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa mtaala wa ngazi hii unatekelezwa kama ulivyoandaliwa.
- Kutoa elimu ya mitaala iliyoboreshwa kwa watekelezaji wote wa mitaala katika eneo lako (wawezeshaji).
- Kusaidia kutoa elimu juu ya Tahasusi.
- Kuhamasisha MEWAKA katika Mikoa/Halmashauri zetu, matumizi ya Maktaba Mtandao na LMS.
- Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mitaala ili kujiridhisha kuwa inatekelezwa kama ilivyopangwa.

# Maboresho ya Mitaala Elimu ya Ualimu

- Utekelezaji wa mitaala ya Ualimu wa Elimu ya Awali, Msingi na Maalumu umeanza Septemba, 2024.
- **Sifa ya kujiunga na ngazi hii ni:**
  a) Elimu ya Sekondari Hatua ya Juu (Kidato cha 6).
  b) Cheti cha Ualimu cha Astashahada
  c) Kidato cha Nne kwa programu ya miaka mitatu kwa masomo ya Sayansi na Hisabati
- Walimu tarajali wa sekondari ni wahitimu wa Shahada ya Elimu ya Juu.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu...

- Mabadiliko ya mitaala ya Ualimu yamelenga kumwandaa mwalimu tarajali:
  - ✓ Mwenye uwezo wa kumfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji.
  - ✓ Kufundisha na kupima maendeleo ya mwanafunzi kwa kuzingatia Stadi za Karne ya 21.
- Mitaala ya elimu ya ualimu imeboreshwa ili iakisi mabadiliko katika mitaala ya shule za awali, msingi na sekondari.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu...

- Maboresho haya yapo katika maeneo ya msingi yafuatayo:
  - **Maudhui ya masomo anayofundisha**: Mwalimu tarajali atapata umahiri wa masomo atakayofundisha kupitia elimu yake kabla hajajiunga na mafunzo ya ualimu.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu…

- **Usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji**: Umahiri huu utapatikana kupitia masomo ya;
  - Saikolojia ya elimu kwa rika husika;
  - Sosholojia ya elimu;
  - Mbinu za kuwasiliana kwa rika husika; mafunzo ya maadili na weledi; na
  - Uwezo wa kuendesha mafunzo.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu…

- **Mbinu za kufundishia**:
  - ✓Mbinu mahsusi kwa somo husika
  - ✓Matumizi ya TEHAMA, teknolojia nyingine saidizi na ufaraguzi (*improvisation*) katika ufundishaji na ujifunzaji.
  - ✓Uchopekaji wa masuala mtambuka katika masomo bebezi.
  - ✓Uelewa wa masuala jumuishi katika ufundishaji na ujifunzaji.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu…

- ✓ Umahiri katika kumjengea mwanafunzi Stadi za Karne ya 21.
- ✓ Umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa madarasa makubwa kwa ufanisi.
- ✓ Umahiri wa kutumia michezo kama nyenzo muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya awali.
- ✓ Umahiri wa kumjengea mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo kama mtaala wa ujenzi wa umahiri unavyoelekeza.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu…

- Ili kuwezesha ufanisi katika mawasiliano mwalimu tarajali:
  - ✓Atafundishwa katika lugha ambayo atafundishia.
  - ✓Tumeanzisha somo jipya la lazima linalotilia mkazo kujenga uwezo wa kuwasiliana kitaalamu *(Professional Communication for Teachers)* katika lugha watakayotumia kufundishia.

# Maboresho katika mitaala ya Elimu ya Ualimu…

## Mbinu za upimaji:

Mwalimu tarajali atafundishwa mbinu za upimaji endelevu na tamati unaozingatia ujenzi wa umahiri pamoja na kukuza Stadi za Karne ya 21.

- Kwa ujumla, Mtaala wa Elimu ya Ualimu umeweka msisitizo kwenye kumjengea mwalimu tarajali umahiri katika mbinu za kufundishia na ualimu kwa vitendo.

# Maeneo ya ujifunzaji na Masomo ya Stashahada ( Elimu ya Awali)

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|
| Misingi ya Kinadharia (*Theoretical foundations of the teaching Profession)* | Falsafa na Maadili ya Ualimu<br>Saikolojia na Sosholojia ya Elimu<br>Mitaala na Ufundishaji<br>Upimaji na Tathamini |
| Ualimu kwa Vitendo | Ualimu kwa Vitendo |
| Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji | Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa mahiri husika |
| Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |

# Maeneo ya ujifunzaji na Masomo ya Stashahada (Elimu ya Msingi)

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|
| Misingi ya Kinadharia | Falsafa na Maadili ya Ualimu<br>Saikolojia na Sosholojia ya Elimu<br>Mitaala na Ufundishaji<br>Upimaji na Tathamini |
| Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya Lugha, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sayansi, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Hisabati, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sayansi Jamii, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Sanaa na Michezo na Ualimu kwa Vitendo |
| Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |

# Maeneo ya ujifunzaji na Masomo ya Stashahada (Elimu Maalumu)

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo |
|---|---|
| Misingi ya Kinadharia | Falsafa na Maadili ya Ualimu, Saikolojia na Sosholojia ya Elimu,Mitaala na Ufundishaji<br>Upimaji na Tathamini |
| Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji | Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye uziwi, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa akili, Mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa mwanafunzi mwenye usonji<br>Ualimu kwa Vitendo |
| Masomo ya Jumla | Elimu Jumuishi |
| Lugha na Mawasiliano | Mawasiliano ya Kitaaluma kwa Walimu |

# Maboresho ya Mitaala Elimu ya Ualimu…

- Ili kuimarisha umahiri na weledi, wahitimu wote wa programu za ualimu watafanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu (*internship*) kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla hawajapewa leseni ya kufundisha.

# Wajibu wa Mthibiti Ubora...

- Kusimamia utekelezaji wa mtaala wa ngazi hii ili kuhakikisha kuwa unatekelezwa kama ulivyoandaliwa.
- Kufuatilia juu ya uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia (Vitabu, mitaala, mihtasari) na kama havipo kuwasiliana na mamlaka husika.

# HITIMISHO

- Shukurani kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
- TET imetoa mafunzo kwa walimu juu ya matumizi ya Maktaba Mtandao na LMS. Hivyo, tunawaomba kusaidia kuhimiza matumizi yake kwa walimu na wanafunzi.
- TET inaendelea kuomba ushirikiano wa karibu kati yake na wathibiti ubora.

# Asanteni kwa Kunisikiliza